

Kuchunguza Lugha Isiyostaha katika Hotuba za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Nchini Tanzania

Nashukuru G. Sanga (Assistant lecturer) na Peter T. Mramba (Ph.D)

Idara ya lugha

Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Morogoro, Tanzania

Baruaapepe: mrambadoctor@gmail.com

Simu: +255 763 090 215 / 785 678 465

IKISIRI

Makala haya yalikusudia kuchunguza lugha isiyostaha ilivyojitokeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Lengo la Makala haya ni kubainisha lugha isiyostaha ilivyojitokeza katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Lengo la kubainisha lugha isiyostaha katika kampeni liliongozwa na Nadharia ya Staha ya mwaka 1981 inayohusishwa na Fraser na Nolen, inayosema kwamba kila taasisi ina miongozo na kanuni inayoeleza ni lugha ipi ina staha na lugha ipi isiyostaha, kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343). Kwa hiyo, katika muktadha wa kampeni, lugha isiyostaha ilikuwa ile inayokiuka maadili ya uchaguzi yaliyowekwa na Tume. Data za utafiti huu zilipatikana maktabani katika mtandao wa YouTube. Mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ndio iliyotumika kukusanya data, kisha data hizo zilichambuliwa kiuelezi, ambapo imebainika kuwa lugha isiyostaha ilivyojitokeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania ni: lugha inayodhalilisha, inayoeleza tuhuma zisizothibitika, inayoonesha kutotii maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, lugha yenyе kebehi, matusi, kashfa, uchochezi, kuzungumza mambo binafsi ya mgombea mwingine hadharani na lugha za jamii. Makala haya yanahitimisha kuwa hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania zilisheheni lugha isiyostaha ambayo kulingana na muktadha wa kampeni za uchaguzi ilikuwa inatumika kwa lengo la kushawishi wapiga kura. Aidha, Makala haya yanashauri utafiti mwingine unaweza kufanyika kuchunguza athari za lugha isiyostaha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Utangulizi

Kampeni ya uchaguzi ni moja ya shughuli za kisiasa na ni njia ya kuwasiliana na wapigakura ambapo wanasiasa hunadi sera zao na vyama vyao (Wei, 2001). Kampeni hizi hufanywa kwa kuanzia mikutano ya ndani ya chama na hatimaye mikutano ya nje na makongamano. Ili kufanikisha kampeni hizi, wagombea huwa wanaandaa matangazo, hotuba, mahojiano na kusambaza majorida, mabango, vitabu, picha na vipeperushi. Yote haya huwasilishwa kwa njia ya lugha. Kimsingi, lugha huchukua nafasi kubwa katika kampeni za uchaguzi kwa sababu ndio nyenzo inayotumika kuwashawishi wapigakura. Kwa hiyo, wanasiasa hutumia lugha kwa namna tofautitofauti wanaponadi sera zao ili waweze kutimiza malengo yao na kukubalika kwa wapigakura wao.

Istilahi Muhimu

Kampeni: *Kampeni ya uchaguzi ni moja ya shughuli za kisiasa na ni njia ya kuwasiliana na wapigakura ambapo wanasiasa hunadi sera zao na vyama vyao (Wei, 2001).*

Lugha ya staha: *Ni lugha inayozingatia kanuni na masharti ya maafikiano ya kimazungumzo.*

(Fraser na Nolen; 1981 na Fraser 1990).

Lugha isiyostaha: *Lugha isiyostaha ni ile ambayo ina kebehi, maudhi, kejeli, matusi na inayodhalilisha watu wengine (Tume ya Uchaguzi; 2020).*

Usuli wa Tatizo

Mchakato wa kampeni nchini Tanzania hutawaliwa na huongozwa na sheria, katiba na maadili ya uchaguzi kwa wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani. Kwa mfano, mwongozo wa maadili uliotolewa na Tume ya Uchaguzi (2020) unasisitiza matumizi ya lugha nzuri ya staha isiyo ya kebehi, kejeli na matusi. Kwa mujibu wa maelezo ya Tume ya Uchaguzi, lugha ya staha katika kampeni ni ile ambayo haina kebehi, kejeli, matusi kwa watu wengine wakiwamo wagombea. Lugha ya staha ndiyo inayosisitizwa katika kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa Mwongozo wa Tume ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo, matumizi sahihi ya lugha katika kampeni za uchaguzi ni suala muhimu ambalo linapaswa kuzingatiwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, tarehe 15 Septemba 2020 inadai kwamba



kulikuwa na matumizi ya lugha isiyostaha kwa baadhi ya wagombea. Lugha isiyostaha ni ile ambayo ina kebehi, maudhi, kejeli, matusi na inayodhalilisha watu wengine.

Hata hivyo, licha ya kuwapo kwa lugha isiyostaha katika misimu tofautitofauti ya kampeni nchini Tanzania ukiwamo wa 2020, tafiti zilizoshughulikia matumizi ya lugha kwenye kampeni, hazikujihusisha na lugha isiyostaha kwa umahususi wake. Kwa mfano, Chalamila (2011) alichunguza uchanganyaji na ubadilishaji msimbo katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 huku mifano ikitolewa kutoka wilaya ya Mufindi kwa kubainisha aina ya ubadilishaji msimbo iliyojitokeza zaidi katika kampeni na sababu za kutokea kwake. Pia, Sovu (2018) alichunguza matumizi ya tamathali za semi za Kiswahili katika kampeni za kisiasa huku akitoa mifano kutoka Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, 2015. Aidha, alibaini kwamba wanasiasa walitumia tamathali za semi mbalimbali kama vile kinaya, sitiari, mdokezo, tashibiha na taashira kwa lengo la kushawishi, kuwaamsha wasikilizaji na kuwavuta katika chama chao ili wapate madaraka.

Sovu (2020) alichunguza matumizi ya lugha katika kampeni za uchaguzi kwa kujishughulisha na mbinu za kisarufi na kibalagha katika vilongo teule vya kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 nchini Tanzania. Katika uchunguzi huo alibaini kwamba mbinu hizo hutumika kwa lengo la kushawishi wapigakura wao. Kwa upande wa lugha isiyostaha Sovu anasema:

Kuna madai kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa maadili kwa baadhi ya wagombea ya kutumia lugha ya matusi na isiyostaha wakati wa kampeni katika ngazi mbalimbali. Hata hivyo, utafiti huo haukujishughulisha kuangalia matumizi sahihi ya lugha wala ukiukwaji wa maadili (Sovu, 2020: 2).

Dondoo hili linadokeza kuwapo kwa lugha isiyostaha kwenye kampeni. Hata hivyo, Sovu haukujishughulisha nayo kwa kuwa halikuwa lengo lake. Mazingira kama haya ndiyo yaliyomvutia mtafiti kuchunguza lugha isiyostaha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Uchunguzi huu ulilenga kufahamu lugha isiyostaha iliyojitokeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Pamoja na lugha isiyostaha kujitokeza katika misimu tofauti ya hotuba za kampeni za uchaguzi mkuu nchini Tanzania, bado suala hili lilikuwa halijapewa umuhimu wa kiuchunguzi. Lugha isiyostaha imeendelea kutumika hata katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyoiezwa katika Taarifa ya Tume ya Uchaguzi ya Tanzania iliyotolewa tarehe 15 Septemba 2020. Kutohakana na lugha isiyostaha kujitokeza katika misimu tofauti ya uchaguzi, watafiti walitaka kufahamu lugha isiyostaha iliyotumika katika kampeni mbalimbali za uchaguzi nchini Tanzania hasa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Staha. Nadharia ya Staha ilitumika kuongoza ubainishaji wa lugha isiyostaha katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania. Nadharia ya Staha inahusishwa na mawazo ya Fraser na Nolen (1981). Kwa mujibu wa Fraser na Nolen (1981) na Fraser (1990), lugha yenye staha ni ile inayozingatia kanuni na masharti ya maafikiano ya kimazungumzo. Wanaendelea kueleza kuwa kila jamii au taasisi imejiwekea kanuni na miongozo inayobainisha kauli gani au uzungumzaji upi unafaa au haufai.



Kwa kuzingatia maelezo ya Fraser na Nolen (1981), lugha yenye kuzingatia kanuni na miongozo ya kijamii au kitaasisi ni ile yenye staha na ile ambayo haizingatii kanuni na miongozo hiyo ni lugha isiyostaha. Mathalani, lugha isiyostaha kwa wagombea kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya

343) ilikuwa ile yenye kutumia matusi, inayodhalilisha wagombea au makundi mengine, yenye kudhifikasi sera za wagombea wengine, yenye kutisha au kutotii maelekezo ya Tume.

Kwa hiyo, katika kubainisha lugha isiyostaha iliyojitekeza katika hotuba za kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania, watafiti waliongozwa na Nadharia ya Staha (1981) inayosema kwamba kila taasisi ina miongozo na kanuni zinazoleza ni lugha ipi ina staha na lugha ipi isiyostaha, kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343). Kulingana na maelezo hayo, lugha ambayo ilikiuka maadili hayo ya uchaguzi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania, ndio ilichukuliwa kama lugha isiyostaha.

Utafiti huu uliongozwa na mawazo ya msingi ya nadharia hii kwamba lugha inaweza kuchunguzwa maana yake kwa kuhusisha muktadha wa matumizi. Kwa hiyo, watafiti baada ya kupata lugha isiyostaha katika hotuba teule za kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania, walichunguza maana zake kulingana na muktadha wa matumizi katika kampeni za uchaguzi.

Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Dhana ya ukusanyaji wa data katika utafiti inahusiana na kitendo cha kukusanya taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti (Ponera, 2019). Anaendelea kueleza kuwa taarifa hizo husaidia kujibu, kufafanua, au kudokeza jambo lolote linalohusiana na malengo ya utafiti. Kwa kuwa utafiti huu unahu kuchunguza lugha isiyostaha iliyojitekeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania, mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ilitumika kukusanya taarifa ambazo zilisaidia kufafanua malengo mahususi ya utafiti huu.

Uchambuzi wa nyaraka ni mbinu inayohusisha uchanganuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na hotuba na maudhui hayo yanaweza kuwa katika maandishi au mazungumzo (Kothari, 2009). Ili kupata data kuhusu lugha isiyostaha katika hotuba za kampeni, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa hotuba hizo zilizopakuliwa katika mtandao wa *Youtube*. Mtafiti alichambua hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania ili kupata taarifa kuhusu lugha isiyostaha iliyotumika katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Lugha Isiyostaha katika Hotuba za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Nchini Tanzania

Sehemu hii inajibu swali la kwanza lilouliza: “lugha isiyostaha iliyojitekeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania ilikuwa ipi?” Katika kujibu swali hili, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Staha mwaka (1981) inayosema kwamba

kila taasisi ina miongozo na kanuni inayoeleza ni lugha ipi ina staha na lugha ipi isiyostaha, kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343) ambapo lugha iliyokuwa inakiuka maadili hayo, ndiyo iliyochukuliwa kama lugha isiyostaha. Kwa kuzingatia nadharia hiyo, majibu ya swali hili yanaonesha kwamba kulikuwa na matumizi ya lugha isiyostaha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1 hapa chini.



Jedwali Na.1: Lugha Isiyostaha Iliyojitokeza katika Hotuba za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Nchini Tanzania

Na.	Lugha Isiyostaha	Hotuba Iliyotumia Lugha Isiyostaha
1.	Lugha inayodhalilisha	Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Mbeya Mjini na Musoma Mjini
2.	Lugha inayoeleza tuhuma zisizothibitika	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia AA, Tabora Mjini na Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Iringa Mjini
3.	Lugha inayoonesha kutotii maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Mbeya Mjini na Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Singida Mjini
4.	Lugha ya kebehi	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Katoro na Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia AA, Airport ya Zamani-Mbeya
5.	Lugha ya matusi	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Singida Mjini na Ikungi
6.	Lugha ya kashfa	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Ikungi, Iringa Mjini, Moshi Mjini na Morogoro Mjini

7.	Lugha ya uchochezi	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Singida Mjini na Tibirizi
8.	Lugha yenye kuzungumza mambo ya mgombea mwingine hadharani	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Tibirizi
9.	Matumizi ya lugha za kijamii	Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia AA, Geita Vijijini

Chanzo: Watafiti (2022)

Sehemu inayofuata inafafanua zaidi lugha isiyostaha iliyobainishwa katika Jedwali Na. 1 ilivyojitekeza katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

1.1 Lugha Inayodhalilisha

Udhalilishaji ni hali ya kumfanya mtu kuwa duni au mnyonge (Torres na Bergner, 2010; Walker na Knauer, 2011; Otten na Jonas, 2014). Kulingana na fasili hiyo, lugha inayodhalilisha ni ile inayomfanya mtu au taasisi kuwa duni, dhalili au mnyonge kinyume na uhalisia wake. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (b) kinamtaka mgombea kutotumia lugha inayodhalilisha mtu, kundi fulani, au taasisi. Data inabainisha kuwa kulikuwa na matumizi ya lugha inayodhalilisha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Tazama Data Na. 1A-B kwa ufanuzi zaidi;

Data Na. 1A

...Tumeingia katika historia ya nchi yetu ambayo AA ya (anamtaja jina) haiwezi tena ushindani wa uchaguzi. Ndiyo maana wanategemea ushindi wa mezani wa Tume ambayo ameichagua yeche mwenyewe. **Anawaambia mkipitisha wapinzani hamna kazi.** AA imefilisika kiasi hicho...

(Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Kupitia BB-Mbeya Mjini²)

Data Na. 1A inabainisha kuwa mgombea urais kupitia BB alitumia lugha inayodhalilisha. Kwa mfano, mgombea anasema: *anawaambia (Tume) mkipitisha wapinzani hamna kazi.* Kwa kuzingatia muktadha wa hotuba ya mgombea urais kupitia BB alimaanisha kwamba Tume ni duni kwani inatishwa na mgombea urais kupitia AA. Maelezo kwamba Tume inatishwa na mgombea urais kupitia AA yanaidhalilisha Tume. Kwa sababu Tume kwa mujibu wa Ibara ya 74 ibara ndogo ya 7, 11, 12 na 14 ni huru. Inafanya kazi bila kutishwa na mtu yeoyote, chama chochote wala mgombea yeoyote. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kusema kwamba mgombea urais kupitia AA anaitishia Tume kwamba wakipitisha wapinzani hawana kazi ni kuidhalilisha Tume. Lugha inayodhalilisha ni lugha isiyostaha kwa sababu inakiuka Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

Kadhalika, Data Na. 1B inabainisha kuwa kulikuwa na matumizi ya lugha inayodhalilisha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na. 1B

...Sasa tumesikia njama zao wanasema hivi watapeleka mawakala wa AA waliowapa barua zinazooonesha ni BB. Hakitaeleweka! (wanashangilia). Bwana Msajili wa Vyama vya Upinzani, **maana yake anajiita Msajili wa Vyama vya Siasa.** Ukweli ni kwamba ni Mdhibiti wa Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, Bwana Mdhibiti wa Vyama vya Upinzani mawakala wetu wasipoingia kwenye vituo vya kupigia kura hakitaeleweka, hakutakuwa na amani...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Kupitia BB, Musoma Mjini³)

² Hotuba: <https://youtu.be/PF-iqhR6G20>

³ Hotuba: <https://youtu.be/FQA5BjlvoOM>

Data Na. 1B inabainisha kwamba mgombea urais kupidia BB alitumia lugha inayodhalilisha. Kwa mfano, mgombea urais kupidia BB anasema *maana yake anajifanya Msajili wa Vyama vya Siasa ukweli ni kwamba ni Mdhibiti wa Vyama vya Upinzani*. Kwa hiyo, *Bwana Mdhibiti wa Vyama vya Upinzani mawakala wetu wasipoingia hakitaeleweka*. Kitendo cha mgombea urais kupidia BB kumwita Mdhibiti wa Vyama vya Upinzani badala ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni kuidhalilisha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Kwa sababu Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imejikita katika usimamizi wa Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya Mwaka 1992, na Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2010 ili kuhakikisha

uwepo na ukuaji wa demokrasia ya vyama vingi nchini⁴. Lugha anayoitumia mgombea urais kupidia BB ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.2 Luga Inayoeleza Tuhuma Zisizothibitika

Tuhuma ni shaka hasi juu ya jambo fulani (Pelkmans, 2018). Kwa kuzingatia fasili ya hiyo, lugha inayoeleza tuhuma zisizothibitika ni ile ambayo inatoa shaka hasi juu ya jambo ambalo halina ushahidi. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (h) kinawataka wagombea kuepuka kutoa tuhuma zisizothibitika. Data inabainisha kuwa kulikuwa na lugha yenye tuhuma zisizothibitika katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Tazama Data Na. 2A-B kwa ufanuzi zaidi.

Data Na. 2A

... Watoto msikubali vurugu, msikubali vurugu wajukuu zangu. **Hawa upinzani wanataka vurugu.** Watoto mnapenda vurugu (hapana). Mnapenda ngumi (hapana). Mnapenda vita (hapana)...
(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Ubunge Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia AA, Tabora Mjini⁵)

Data Na. 2A inabainisha kwamba mgombea ubunge kupidia AA alitumia lugha yenye tuhuma zisizothibitika. Kwa mfano, mgombea huyo anasema *hawa wapinzani*

⁴ <https://www.orpp.go.tz>

⁵ **Hotuba:** <https://youtu.be/CEwdE1EKu6c>

wanataka vurugu. Kitendo cha kutamka maneno hayo ni kutoa tuhuma zisizothibitika kwa upande wa vyama vya upinzani. Ukweli ni kwamba vyama vya upinzani kama vile BB katika uchaguzi mkuu havikuwa vinataka vurugu bali Tanzania yenyе Uhuru, Haki na Maendeleo ya Watu⁶. Pia, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi aliripoti kuwapo kwa wagombea wanaotoa tuhuma zisizothibitika (taz. https://youtu.be/B-7aP81_-B0). Kwa hiyo, katika muktadha wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania, kutumia lugha yenyе tuhuma zisizothibitika ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (h) cha Maadili ya Uchaguzi.

Kadhalika, Data Na. 2B inabainisha kuwa kulikuwa na lugha yenyе tuhuma zisizothibitika katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na.2B

...Fikirieni nyie hapa ni zaidi ya laki na kila mmoja amekuja kwa hiari yake. **Ukiangalia mikutano yote ya (anamtaja jina) asipohonga elfu tano tano watu hawaendi** asipopeleka matrekta watu hawaendi. Asipopeleka malori watu hawaendi. Asipopeleka magari watu hawaendi. Kwa sababu wanajua viongozi wa AA si viongozi wao tena (wanashangilia)...
(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Iringa Mjini⁷)

Data Na. 2B inabainisha kwamba mgombea urais kupitia BB alitumia lugha yenyе tuhuma zisizothibitika. Kwa mzano, mgombea anasema *ukiangalia mikutano yote ya (anamtaja jina) asipohonga elfu tano tano watu hawaendi*. Kusema kwamba mgombea wa AA asipohonga elfu tano tano katika mikutano yake yote watu hawaendi ni kutoa tuhuma isiyothibitika. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa video za *Youtube* idadi ya watu waliokuwa wanaonekana katika mikutano ya mgombea huyo wa urais kupitia AA haingekuwa rahisi kumhonga kila mtu elfu tano tano⁸. Pia,

⁶ **ILANI YA BB:** <https://chadema.or.tz/wp-content/uploads/2020/09/ILANI-YA-CHADEMA-2020-2025.pdf>

⁷ **Hotuba:** <https://youtu.be/Wfe4yx-9vTc>

⁸ **TAZAMA IDADI YA WATU KATIKA MKUTANO WA MGOMBEA UR AIS KUPITIA AA UWANJA WA KAMBARAGE -SHINYANGA:** <https://youtu.be/70uQLnXhHml>

chama ambacho kimekuwapo madarakani kwa miongo zaidi ya miwili si rahisi kupoteza wanachama kiasi cha kuhonga kila mtu ndipo watu washawishike kwenda kwenye kampeni. Kwa hiyo, kutumia lugha yenye tuhuma zisizothibitika katika hotuba za kampeni ni lugha isiyostaha kwani inakwenda kinyume na Kifungu Na.

2.2 (h) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.3 Luga Inayoonesha Kutotii Maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kutii ni kitendo cha kufanya ulivyoamriwa au kufuata amri (TUKI, 2019). Kwa kuongezea kwenye fasili ya TUKI, kutii ni kitendo cha kufanya au kufuata amri, maelekezo au maagizo yaliyotolewa na mamlaka katika muktadha husika. Kwa mfano, kwenye muktadha wa uchaguzi wenyе mamlaka ni Tume ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.1 (a) kinawataka wagombea kufuata maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa kuzingatia maadili haya, lugha yoyote inayotumiwa na wagombea inayoonesha kutotii maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania, ni lugha isiyostaha. Data inabainisha kuwa kulikuwa na lugha inayoonesha kutotii maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Tazama Data Na. 3A-B kwa ufanuzi zaidi.

Data Na.3A

...Hatuwezi kurudi enzi ambazo bajaji na bodaboda wanazuiliwa kupita kwenye barabara ambazo mbunge wao ndiyo anazitetea. Hatuwezi kurudi nyuma na **tutapiga kura, tutalinda kura na tutakomaa hadi mwisho...**

(Hotuba ya Kampeni ya Mgomea Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Kupitia BB, Mbeya Mjini⁹)

Data Na. 3A inabainisha kuwa lugha aliyoitumia mgombea ubunge kupitia BB haitii maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mathalani, mgombea ubunge kupitia BB anasema: *tutapiga kura, tutalinda kura na tutakomaa mpaka mwisho*. Kauli hiyo

⁹ **Hotuba:** <https://youtu.be/Z6s-28DDLa4>

inamaanisha kwamba wapigakura pindi watakapopiga kura katika vituo husika wasiondoke vituoni hadi mwisho wa zoezi. Hata hivyo, maelekezo anayotoa mgombea ubunge kupitia BB kwa wanachama wake ni kinyume na maelekezo ya Tume ya Taifa kwa mpigakura. Kwa sababu Tume ya Taifa inasema: *viongozi wa vyama vya siasa watawaelimisha na kuwaasa wanachama wao kuwa, mara wanapomaliza kupiga kura waondoke vituoni ili kuepusha msongamano na vitendo vinavyoweza kuchochea uvunjifu wa amani.* Kwa hiyo, kitendo cha mgombea ubunge kupitia BB kusisitiza wapigakura kubaki vituoni baada ya kupiga kura hadi mwisho ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.1 (a) cha Maadili ya Uchaguzi.

Kadhalika, Data Na. 3B inabainisha kuwa kulikuwa na lugha inayoonesha kutotii maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na. 3B

...Msiogope. Mkatimize wajibu wenu. Msiogope. Mnaniptata (ndiyo) mkalinde kura. Ukipiga kura subiri hesabu yako. **Usipige kura ukaenda nyumbani. Wezi wataiba.** Mnaniptata (ndiyo). Tukapige kura tusubiri hesabu yetu. Tulinde kura isiibiwe na Manyang"au. Mnaniptata eeh (ndiyo)...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Singida Mjini¹⁰)

Data Na. 3B inabainisha kuwa mgombea urais kupitia BB alitumia lugha inayoonesha kutotii maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mfano, mgombea urais kupitia BB *anasema: usipige kura ukaenda nyumbani. Wezi wataiba.* Maelekezo haya yanayotolewa na mgombea urais kupitia BB kwa wanachama wake kwamba pindi watakapokuwa wametekeleza shughuli ya kupiga kura wasirudi nyumbani ni kinyume na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa maelekezo ya Tume, mpiga kura akishapiga kura anapaswa kuondoka kituoni ili kuepusha msongamano na vitendo vinavyoweza kuchochea uvunjifu wa amani. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kuhimiza

¹⁰ **Hotuba:** <https://youtu.be/CLTSdyZHLnk>

wapigakura kutorudi nyumbani baada ya kupiga kura ni lugha isiyostaha kwa sababu inakiuka Kifungu Na. 2.1 (a) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.4 Lugha ya Kebehi

Kebehi ni maneno ambayo kijuujuu yanasi kika vizuri masikioni wakati huo huo maneno hayo hukusudia kutoa maana ambayo ni kinyume chayo kabisa (Senkoro,

1982). Maneno ya kebehi mara nyingi kwa undani wake huwa yanaudhi hususani kwa yule anayekebehiwa. Hii ina maana kwamba lengo kubwa la kebehi licha ya kwamba inasemwa kimasihara ni kumkera mtu au kumcheka mtu kwa namna ambayo inamfanya achukie. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (b) kinamtaka mgombea kutotumia lugha ya kebehi kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni. Kwa kuzingatia maadili haya, lugha yoyote inayooneshwa kukebehi katika shughuli za mikutano na kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania ni lugha isiyostaha. Data inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yenyе kebehi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 4A-B.

Data Na. 4A

...Lini mliwahi kuona watu wanatekwa nyara na kupotezwa kama miaka mitano ya (anamtaja jina). Nani aliwahi kuona (hatujawai). Hamjawahi kuona siyo. Hii ndiyo maana wanasema wametekeleza kwa kishindo. **Wametekeleza mauaji kwa kishindo. Wametekeleza mateso kwa kishindo.** Wameharibu uchumi wa nchi hii...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Katoro¹¹)

Data Na. 4A inabainisha kwamba mgombea wa urais kupitia BB alitumia kebehi katika hotuba yake wakati wa kampeni. Kwa mfano, mgombea anasema: *hii ndiyo maana wanasema wametekeleza kwa kishindo. Wametekeleza mauaji kwa kishindo. Wametekeleza mateso kwa kishindo.* Lugha hii ni kebehi kwa AA ambao walikuwa na kaulimbiu inayosema: *Tumetekeleza kwa Kishindo, Tunasonga Mbele Pamoja.*

Kaulimbiu hii haikuwa na maana kwamba wametekeleza kwa kishindo mauaji na

¹¹ Hotuba: <https://youtu.be/QaTR7tUy3HY>

mateso kama anavyosema mgombea wa kitit cha urais kupidia BB. Ilikuwa na maana kwamba wametekeleza ilani yao ya 2015 vizuri ambayo ililenga kuinua uchumi wa nchi. Kitendo cha mgombea huyo kuhusisha mauaji na mafeso kama moja ya mambo ambayo AA wameyatekeleza kwa kishindo ni kukikebehi chama hicho. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupidia BB kukebehi kaulimbiu ya AA ya mwaka 2015 katika hotuba yake wakati wa kampeni ilikuwa lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

Pia, Data Na. 4B inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yeny kebehi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na. 4B

...Nileteeni Tulia. Hilo ndilo likawe la kwanza kushughulikiwa. Kwa sababu **mlikosa msemaji, mlipata msanii**. Msanii wakuwadanganya sio msanii mzuri kama Diamond na Ali Kiba... (Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia AA, Airport ya Zamani¹²).

Data Na. **4B** inabainisha namna mgombea urais kupidia AA alivyotumia kebehi kwa mgombea ubunge kupidia BB, jimbo la Mbeya Mjini ambaye alikuwa mbunge wa awamu iliyopita. Kwa mfano, mgombea anaposema: *mlikosa msemaji, mlipata msanii*. Lugha hii inaonesha kwamba jimbo lililokuwa linaongozwa na mbunge wa BB lilikosa msemaji kwa sababu mbunge huyo hakuwa na sifa ya kuwa msemaji bali msanii, si tu msanii bali msanii mdanganyifu. Lugha hii ingawa ilisemwa kimasihara ni lugha ya kuudhi. Kwa sababu kusema kwamba jimbo lilikosa msemaji bali lilipata msanii ni sawa na kusema jimbo lilikuwa na msemaji mwongo.

Hivyo, kitendo cha mgombea urais kupidia AA kusema hadharani kwamba wananchi wa Mbeya Mjini hawakupata msemaji bali walipata msanii mdanganyifu ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inamkebehi mbunge wa awamu ya tano kupidia BB jimbo la Mbeya Mjini kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya

Uchaguzi.

¹² **Hotuba:** <https://youtu.be/ET6aNAQF078>

1.5 Lugha ya Matusi

Matusi hujumuisha tabia au mazungumzo ya mdomo au maandishi ambayo humnyanyasa mtu, na wakati mwingine hukusudia kudharau, kufedhehesha na kuudhi (Gabriel, 1998). Naye Ivanishcheva na wenzie (2018) wanaeleza kuwa matusi ni lugha inayobainisha unyonge wa mtu au uelezaji wa jambo kwa namna isiyofaa. Aidha, kwa upande wa mila na desturi za Watanzania matusi hurejelewa kama kutenda mambo ambayo ni mwiko kulingana na imani, mzaoea au tabia. Kwa ujumla, katika Makala haya tunachukulia kuwa matusi ni lugha inayoonesha dharau, kufedhehesha na kuudhi. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (b) kinamtaka mgombea kutotumia lugha ya matusi kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni. Data inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yenye matusi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 5A-B.

Data Na. 5A

...Leo hii imekuwa rahisi kumkosoa Mungu kuliko kumkosoa (anamtaja jina).

Nasema uongo (hapana). Kama unabisha waulize masheikh wa mkoa huu...

(Hotuba za Kampeni za Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Kupitia BB, Singida Mjini¹³)

Data Na. 5A inabainisha namna mgombea urais kupitia BB alivyotumia lugha ya matusi kwa mgombea kiti cha urais kupitia AA. Lugha inayodhihirisha matusi hayo ni: *leo imekuwa rahisi kumkosoa Mungu kuliko kumkosoa (anamtaja jina)*. Lugha hii ni matusi kwa mgombea huyo kwani kulingana na muktadha huu, ina maana kwamba mgombea urais kupitia AA anajiona mkamilifu kama Mungu. Kwa mujibu wa imani ya mgombea urais kupitia AA, maneno hayo hangeyapokea vizuri, yaani yengemuudhi. Halikadhalika, kulingana na utamaduni wa Mtanzania ni matusi makubwa mtu yoyote kujifananisha na Mungu kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kusema ni rahisi kumkosoa Mungu

¹³Hotuba: <https://youtu.be/CLTSdyZHLnk>

kuliko mgombea urais kupidia AA ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

Pia, Data Na. 5B inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yeny matusi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na. 5B

...Tumekuwa tunaonewa. Watu wanauwawa. **Jeshi la polisi ambalo linasema wajibu wake ni kulinda raia na mali zake. Hawajawahi kulinda raia amba ni wanachama wa BB...**

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Ikungi¹⁴)

Data Na. 5B inabainisha jinsi mgombea urais kupidia BB alivyowatusi polisi kwenye hotuba yake ya kampeni. Kwa mfano, mgombea anasema: *jeshi la polisi ambalo linasema wajibu wake ni kulinda raia na mali zake, halijawahi kulinda raia amba ni wanachama wa BB*. Lugha hii ni tusi kwa sababu wakati alipokuwa anatoa kauli hiyo, video kupitia *Youtube* ilikuwa inaonesha kulikuwa na jeshi la polisi kama inavyooneshwa katika <https://youtu.be/zzBnvhej>. Hivyo, kitendo cha mgombea urais kupidia BB kusema polisi hawajawahi walinda wanachama wa BB ilhali walikuwa wanawalinda ni matusi, na ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakiuka Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.6 Lugha ya Kashfa

Kashfa ni uwekaji hadharani wa maovu yaliyokuwa yamefichwa hapo awali (Thompson, 2000; Dewberry, 2015). Kwa hiyo, lugha ya kashfa ni ile ambayo inaweka hadharani maovu yaliyokuwa yamefichwa hapo awali. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (b) kinamtaka mgombea kutotumia lugha ya kashfa kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni. Kwa mujibu wa maadili haya, hotuba ya kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yeny lugha ya kashfa ni lugha isiyostaha. Data

inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yeny kashfa katika hotuba za kampeni za

¹⁴ Hotuba: <https://youtu.be/zzBnvhej>

Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 6.

Data Na. 6

...Tangu ameingia madarakani 2015 viongozi wa BB wameuwawa (wengi). Viongozi wangapi wa BB wameshitakiwa kwa kesi za uongo (wengi). Ni wangapi ambao wameharibiwa biashara zao. Ni wangapi ambao wameumizwa kama mimi. Wengi sana...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Ikungi¹⁵)

Data Na. 6 inabainisha kashfa aliyoitoa mgombea urais kupitia BB kwa mgombea wa urais kupitia AA aliyekuwa rais tangu 2015. Kashfa aliyoitoa ni kuweka wazi maovu yaliyokuwa yamefichwa hapo awali kama vile mauaji ya viongozi wa upinzani, kesi za kusingiziwa na kuharibiwa biashara mionganii mwa wananchi. Kwa hali ya kawaida rais, anatakiwa kulinda raia wake na kuhakikisha uchumi unastawi ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya kibashara. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kuongea hadharani kwamba: *mauaji, kesi za kusingiziwa kwa viongozi wa BB na wafanyabiashara kuharibiwa biashara vimeanza kipindi mgombea wa urais kupitia AA alipoingia madarakani mwaka 2015* ni lugha isiyostaha. Kwa sababu lugha hiyo inafunua mambo ya aibu kumhusu mgombea urais kupitia AA, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu Na.2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.7 Lugha ya Uchochezi

Uchochezi ni istilahi inayorejelea kauli zinazosababisha uadui, ubaguzi au vurugu dhidi ya mtu mmoja na mwingine au kundi moja na lingine (United Nations Human Rights, h.m). Kwa mujibu wa Maadili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (b) kinamtaka mgombea kutotumia lugha inayochochea uvunjifu wa amani kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni. Kulingana na maadili haya, lugha yoyote inayochochea uvunjifu wa amani ni lugha isiyostaha. Data inabainisha kwamba kulikuwa na lugha ya uchochezi katika hotuba

15 Hotuba: <https://youtu.be/zzBnvhej>

za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 7A-B.

Data Na.7A

...Mnanipata (ndiyo) na mkalinde kura. Ukipiga kura, subiri hesabu yako. **Usipige kura ukaenda nyumbani. Wezi wataiba.** Mnanipata (ndiyo). Tukapige kura tusubiri hesabu yetu. Tulinde kura isiibiwe na manyang“au... (Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Singida-Mjini¹⁶)

Data Na. 7A inabainisha namna mgombea urais kupitia BB alivyotumia lugha inayochocha uvunjifu wa amani hususani kwenye vituo vya kupigia kura. Kwa mfano, lugha inayochocha uvunjifu wa amani katika hotuba hiyo ni: *Usipige kura ukaenda nyumbani. Wezi wataiba.* Lugha hii inachocha uvunjifu wa amani kwa sababu inamwelekeza mpigakura kutoondoka kituoni baada ya kupiga kura. Hii ni kinyume na maelekezo ya Tume ambayo yanamtaka mpigakura kuondoka kituoni mara baada ya kupiga kura ili kuepusha msongamano unaoweza kusababisha vurugu. Kupishana huko kwa maelekezo kati ya Tume na mgombea urais kupitia BB kunaweza kuleta vurugu katika vituo vya kupigia kura. Hii ni kwa sababu pindi wasimamizi watakapowaamuru wafuasi wa BB waondoke vituoni baada ya kupiga kura, wanaweza kufikiri kuwa wanawaamuru waondoke vituoni ili iwe rahisi kuwaibia kura zao.

Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kutumia lugha inayochocha uvunjifu wa amani kati ya wapigakura na wasimamizi wa uchaguzi ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha ya kichochezi inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

Pia, Data Na. 7B inabainisha kuwa kulikuwa na lugha ya uchochezi katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania.

Data Na. 7B

...Tutajenga muungano wa haki kwa sababu Muungano wa Mwaka 1964 haujawahi kuwa wa haki hata kidogo. **Mahusiano kati ya**

¹⁶ Hotuba: <https://youtu.be/QaTR7tUy3HY>

Zanzibar na Tanganyika tangu mwaka 1964 yamekuwa mahusiano ya kikoloni. Mahusiano kati ya koloni na taifa linalotawala koloni hilo. Hayo ndiyo yamekuwa mahusiano ya Tanganyika na Zanzibar tangu tarehe 26/04/1964 uliposainiwa mkataba wa makubaliano ya Muungano...
 (Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Tibirizi¹⁷)

Data Na. 7B inabainisha lugha ya kichochezi aliyoitumia mgombea urais kupitia BB. Kwa mfano, lugha ya kichochezi ni: *mahusiano kati ya Zanzibar na Tanganyika tangu mwaka 1964 yamekuwa mahusiano ya kikoloni. Mahusiano kati ya koloni na taifa linalotawala koloni hilo.* Lugha kama hii inachochea uvunjifu wa amani kwa wananchi kuanza kufikiri kujitoa kwenye muungano wenye dhuluma. Wananchi ambao wanahutubiwa na mgombea urais kupitia BB ni wa Zanzibar ambapo anaeleza kwamba katika muungano huo Tanzania Bara imeifanya Zanzibar kuwa kama koloni lake. Ndiyo, maana katika hotuba yake anasema mahusiano kati ya Zanzibar na Tanganyika yamekuwa kama koloni na taifa linalotawala koloni hilo. Lugha kama hii inaweza kuchochea machafuko, watu wanaweza kupigana ili kujiondoa kwenye muungano. Kwa hiyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kusema kwamba muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika haujawahi kuwa wa haki kinachochea uvunjifu wa amani kati ya pande hzo mbili. Hii ni lugha isiyostaha kwa sababu inakwenda kinyume na Kifungu Na. 2.2 (b) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.8 Kuzungumza Mambo Binafsi ya Mgombea Mwingine Hadharani

Mambo binafsi ni mambo ya mtu, kundi au taasisi ambayo ni kwa ajili ya taasisi hiyo tu, na kwamba hayapaswi kusemwa hadharani. Kwa mujibu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.2 (h) kinasema kukosoana kati ya vyama na wagombea kunapofanyika inabidi kujikita katika sera, programu na kazi zao walizofanya. Kifungu hiki kinamaanisha kwamba ukosoaji nje ya sera, programu au mambo aliyoyafanya mgombea au chama haukulaliki. Kwa hiyo, mgombea anayemkosoa mgombea mwingine nje ya sera, programu au kazi

¹⁷ Hotuba: <https://youtu.be/DbaY9zG2eKo>

aliyofanya mgombea huyo inachukuliwa kama lugha isiyostaha. Data inabainisha kwamba kulikuwa na lugha yenyenye kuzungumzia mambo binafsi ya mgombea nje ya sera, programu na kazi aliyoifanya katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 8.

Data Na. 8

...(Huyu ambaye ameumiza kila mtu **sasa hivi kwenye kampeni akifanya siku mbili tatu hivi anarudi gereji (hospitali) akakarabatiwe. Akitoka anafanya fanya siku mbili, tatu anarudi gereji akakarabatiwe wakampepee pepee hivi.** Miezi miwili ameshapumzika mara sita. Kwisha! (wanashangilia)...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kupitia BB, Tibirizi¹⁸)

Data Na. 8 inabainisha jinsi mgombea urais kupitia BB anavyosema mambo binafsi ya mgombea urais kupitia AA hadharani. Mambo binafsi yanayozungumzwa hadharani ni: *sasa hivi kwenye kampeni akifanya siku mbili, tatu anarudi gereji (hospitali) akakarabatiwe. Akitoka anafanya fanya siku mbili, tatu anarudi gereji (hospitali) akakarabatiwe. Wakampepee hivi.* Lugha hii ni lugha ambayo inaeleza masuala ya kiafya ya mgombea urais kupitia AA hadharani ilhali haya ni mambo binafsi ya mtu mwenyewe wala hayapaswi kuanikwa hadharani. Mambo yote haya anayoeleza mgombea urais kupitia BB kumhusu mgombea urais kupitia AA ni nje na sera, programu na kazi alizofanya mgombea huyo. Hivyo, kitendo cha mgombea urais kupitia BB kuzungumzia masuala ya kiafya ya mgombea urais kupitia AA ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakiuka Kifungu Na. 2.2 (h) cha Maadili ya Uchaguzi.

1.9 Matumizi ya Lugha za Jamii

Kwa mujibu wa Whiteley (1969) na Batibo (1992), Tanzania kuna lugha za jamii zaidi ya 120 na Kiswahili kikiwamo. Lugha za jamii ni nyingi na kama zingeendelea kutumika zingehatarisha umoja wa kitaifa. Hivyo, Sera ya Lugha ya mwaka 1997

ambayo ilizingatiwa katika Sera ya Utamaduni ilielekeza kuwa Kiswahili pekee

¹⁸ Hotuba: <https://youtu.be/DbaY9zG2eKo>

ndiyo kitumike katika maeneo rasmi ili kujenga umoja wa kitaifa. Hadi leo Kiswahili ndiyo lugha pekee ya kijamii inayotumika katika shughuli rasmi. Nayo Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha

124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343); Kifungu Na. 2.1 (k) kinawataka wagombea kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa lugha pekee inayotumika katika kampeni za uchaguzi. Pale ambapo lugha hiyo haieleweki, na itakapolazimu, mgombea atazungumza kwa Kiswahili na mkalimani atakalimani katika lugha inayoleweka kwa jamii husika. Kwa lugha rahisi ni kwamba mgombea anapaswa kutumia Kiswahili pekee katika kampeni na si vinginevyo. Data inaonesha kulikuwa na matumizi ya lugha za jamii katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania kama inavyooneshwa katika Data Na. 9.

Data Na. 9

...Mheshimiwa Rais mengine niachie na mimi ni mbunge wako mchapa kazi.

Tukulolalola mukaya, tukulima byenekili (Tafsiri yangu) Tutaangalia wenyewe hapa hapa nyumbani na tutayamaliza sisi wenyewe...

(Hotuba ya Kampeni ya Mgombea Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania-Kupitia AA, Geita Vijijini¹⁹)

Data Na. 9 inabainisha jinsi mgombea wa ubunge wa jimbo la Geita Vijijini kupitia AA alivyotumia Kisukuma katika hotuba yake ya kampeni. Lugha ya Kisukuma inadhihirika anaposema: *tukololalola mukaya, tukulimala byenekili (tutaangalia wenyewe hapa hapa nyumbani na tutayamaliza sisi wenyewe)*. Lugha za kijamii kama hii ya Kisukuma haikubaliki katika maeneo rasmi kwa sababu zinahatarisha umoja wa kitaifa. Hii ni kwa sababu kitendo cha kutumia lugha ya kijamii kunachochea ukabila, suala ambalo Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere, alikuwa akilikemea kama anavyoileza katika Hotuba ya Mkutano Mkuu wa CCM Dodoma mwaka 1995 (taz. <https://youtu.be/GAEpisZ3Cuk>). Kwa hiyo, kitendo cha mgombea ubunge kupitia AA katika jimbo la Geita Vijijini kutumia Kisukuma, lugha ambayo haijaruhusiwa kutumiwa na mgombea mahali popote ni lugha isiyostaha. Hii ni kwa sababu lugha hiyo inakiuka Kifungu Na. 2.1 (k) cha Maadili ya Uchaguzi.

¹⁹ **Hotuba:** <https://youtu.be/8zbgwK4THFs>

Hitimisho

Ssehemu hii ya makala imewasilisha na kuchambua data kuhusu lugha isiyostaha katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Uwasilishaji na uchambuzi uliofanyika katika Makala haya ulinua kujibu swali: “lugha isiyostaha iliyojitokeza katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania ilikuwa ipi?” Swali hili lilishughulikiwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Staha mwaka 1981 inayosema kwamba kila taasisi ina miongozo na kanuni inayoeleza ni lugha ipi ina staha na lugha ipi isiyostaha, kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2020 (Chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343). Kwa kuongozwa na maadili hayo, lugha isiyostaha iliyobainika kutumiwa katika hotuba za kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania ni pamoja na lugha inayodhalilisha, inayoeleza tuhuma zisizothibitika, inayoonesha kutotii maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, lugha ya kebehi, matusi, kashfa, uchochezi, lugha yenye kuzungumza mambo binafsi ya mgombea mwingine hadharani na matumizi ya lugha za jamii.

MAREJELEO.

Batibo, H. M. (1992) “The Fate of Ethics Language in Tanzania”. Katika M. Brezinger (Mh.) *Language Death: Factual and Theoretical Exploration with Special Reference to East Africa*. Berlin: Mouton. kur. 85-95.

Chalamila, A. (2011) *Uchanganyaji na Ubudilishaji Msimbo katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka, 2010: Mifano Kutoka Wilaya ya Mufundi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

- Dewberry, D. (2015) *The American Political Scandal: Free Speech, Public Discourse and Democracy*. New York: Roman and Littlefield.
- Fraser, B na Nolen, W. (1981) "The Association of Difference with Linguistics Form". *International Journal of the Sociology of Language*, Juz. 27: 93-109.
- Gabriel, Y. (1998) An Introduction to the Social Psychology of Insults in Organizations". *Human Relations*, Juz. 51(11): 1329-1354.
- Ivanishcheva, O.N., Bolgova, E.V., Shadrina, I.M., Gushchina, A.V. na Nikonorov, S.B. (2018) "Insult as a Linguistics and Legal Phenomenon". *International Journal of Engineering & Technology*, Juz, 7(4:38): 216-219.
- Kothari, C.R. (2009) *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Ltd.
- Otten, M. na Jonas, K.J. (2014) Humiliation as an Intense Emotional Experience: Evidence from the Electro-encephalogram". *Social Neuroscience*, Juz. 9:23-35.
- Pelkmans, M. (2018) "Doubt, Suspicion, Mistrust...Semantic Approximations". *The London School of Economics and Political Science*: 1-12.
- Ponera, P.S. (2019) *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982) *Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Sovu, A.Y. (2018) "Matumizi ya Tamathali za Semi za Kiswahili katika Kampeni za Kisiasa: Mifano Kutoka Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, 2015". *SUMAIT University Journal*, Juz. 4: 1-25.
- Sovu, A.Y. (2020) *Uchanganuzi wa Mbinu za Kisarufi na Kibalagha katika Vilongo Teule vya Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2015, Nchini Tanzania*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Thompson, J. (2000) *Political Scandal: Power and Visibility in the Media Age*. New York: Cambridge University Press.
- Torres, W.J. na Bergner, R.M. (2010) "Humiliation: Its Nature and Consequences". *J Am Acad Psychiatry Law*, Juz. 38: 195-204.
- TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2020) *Mwongozo wa Maadili ya Vyama vya Siasa kwaUchaguzi Mkuu*. Katika www. nec.tz.
- United Nations Human Rights (h.m.) Ukurasa Mmoja Juu ya,,Uchochezi"'. Inapatikana katika https://www.ohchr.org/site/default/files/Rabat_threshold_test_Swahili.pdf. Ilisomwa tarehe 17 Machi 2022.
- Walker, J. na Knauer, V. (2011) "Humiliation, Self-esteem and Violence". *Journal of Forensic Psychiatry and Psychology*, Juz. 22: 724-741.
- Wei, J.M.Y. (2001) "Politeness and Politics: The Shui-Bians rhetorical Strategies".*The Journal of Humanities, National University*, Juz. 83: 1-23
- Whiteley, W. (1969) *Swahili: The Rise of National Language*. London: Me